


TOTO TWIGA
NA NDOTO ZA MWAKA MPYA

TOTO TWIGA'S NEW YEAR DREAMS




Toto Twiga, Leo ni siku ya mwaka mpya.

Je unajua salamu yetu ya mwaka mpya?

- "Ndio. Heri ya kuzaliwa!"

Hapana, umekosea. Jaribu tena.



Toto Twiga, today is new year's day.

Do you know our New Year's greeting?

- "Yes. Happy Birthday!"


No, that's not right. Try again.

Mama Twiga, Mwaka Mpya tunasemaje?

- "Tunasema Heri ya mwaka Mpya!"

Oh! Heri ya mwaka Mpya!

Sasa najua salamu ya mwaka mpya, nitamwambia kila mtu!



Mama Twiga, What do we say on the new year?

- "We say, Happy New Year!"

Oh! Happy New Year!


Now I know the new year's greeting! I will tell everyone!

Toto Twiga na Rafiki yake.

Rafiki yangu Toto Tembo, Heri ya mwaka mpya!

Tutunze mazingira yetu.

Ndoto yangu ya mwaka mpya ni kupanda miti.



Toto Twiga with her friend.

My friend Toto Tembo, Happy New Year!

Let's take care of our environment.

My new year dream is to plant trees.

Toto Twiga na shangazi yake.

Shangazi, Heri ya mwaka mpya!

Mwaka mpya, ndoto mpya.

Ndoto yangu ya mwaka mpya ni kusoma kitabu kipya.



Toto Twiga with her Aunty.

Happy New Year Aunty!

New Year, new dreams!

My new year dream is to read a new book.

Toto Twiga na mjomba wake.

Mjomba, Heri ya mwaka mpya!

Mwaka mpya ndoto mpya!

Ndoto yangu ya mwaka mpya ni kusaidia kazi nyumbani.



Toto Twiga with her Uncle.

Happy New Year Uncle!

New Year, New dreams!


My new year dream is to help with house chores.

Toto Twiga na kaka yake.

Kaka yangu, Heri ya mwaka mpya!

Tujifunze vitu vipya.

Ndoto yangu ya mwaka mpya ni kujifunza kiswahili.



Toto Twiga with her brother.

Happy New Year my brother!

Let's learn new things.

My new year dream is to learn Swahili.

Toto Twiga na dada yake.

Dada yangu, Heri ya mwaka mpya!

Tufanye vitu vipya.

Ndoto yangu ya mwaka mpya ni kuandika kitabu changu.



Toto Twiga with her sister.

Happy New Year my sister!

Let's do new things.

My new year dream is to write my own book.


Toto Twiga na jirani yake.

Jirani yangu, Heri ya mwaka mpya!

Tujenge afya bora.

Ndoto yangu ya mwaka mpya ni kufanya mazoezi.

Kutembea na kukimbia kila siku!



Toto Twiga with her neighbour.

Happy new year my neighbour, let's get healthy.

My new year dream is to be active.

Walking and running everyday!


Toto Twiga na mdogo wake.

Heri ya mwaka mpya mdogo wangu!

Tujifunze tabia njema!

Ndoto yangu ya mwaka mpya ni kusema....

Tafadhali, asante na samahani.



Toto Twiga with her little sister.

Happy New year my little sister!

Let's learn good manners!

My new year dream is to say.....

Please, thank you and sorry.

Toto Twiga na bibi yake.

Heri ya mwaka mpya bibi yangu!

Tutumie vipaji vyetu.

Ndoto yangu ya mwaka mpya ni kuwa kiongozi.



Toto Twiga and her grandmother.

Happy New Year grandma!

Let's use our talents!


My new year dream is to become a leader.

Toto Twiga na babu yake.

Heri ya mwaka mpya babu yangu!

Tujifunze kupika chakula.

Ndoto yangu ya mwaka mpya ni kujifunza kupika pilau.



Toto Twiga and her grandfather.

Happy New Year grandpa!

Let's learn to how make food.

My new year dream is to learn how to make pilau

Toto Twiga na baba yake.

Heri ya Mwaka mpya baba! Tucheze pamoja.

Ndoto yangu ya mwaka mpya ni kucheza na familia.



Toto Twiga and her dad.

Happy New year daddy! Let's play together.

My new year dream is to play with my family.

**Toto Twiga kwa Msomaji.
Heri ya mwaka mpya msomaji!
Nakutakia furaha, amani na upendo!**

**Je, ndoto yako ya mwaka
mpya ni kufanya nini?**



**Toto Twiga to the reader.
Happy new year reader!
I wish you joy, peace and love!
What's your new year's dream?**

ZOEZI

Chagua jibu sahihi - Pick the right answer

Mwaka mpya tunasema?

- a. Shikamoo mwalimu
- b. Heri ya mwaka mpya
- c. Kwaheri mwalimu


Neno upendo kwa kiingereza ni nini?

- a. Happiness
- b. Peace
- c. Love

Neno ndoto lina maana gani kiingereza?

- a. Play
- b. Read
- c. Dream

Toto Twiga Mini Book Series by....



swahiliKIDS

To get more free & fun Swahili Learning resources visit

 <https://www.swahilikids.com/>



@kiswahiliKIDS



@swahiliKIDS



@swahili.KIDS